Njia Ya Mkato Si Mbali Vya Kutosha

na

Ellis P. Forsman

Njia Ya Mkato Si Mbali Vya Kutosha

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 7, 2011

Njia Ya Mkato Si Mbali Vya Kutosha

Mwanzo 11:

Kujifunza Agano la Kale inaweza kuvutia sana. Leo, walimwengu wengi hawaamini kilicho andikwa ndani yake. Wanafikiri ni kitabu kingine cha kufikirika, iliyopitwa na wakati. Hawazingatii kwamba mkono wa Mungu uliongoza maandishi haya, hivyo lazima tuvichukue vyote kuwa kweli.

Waru. 15:4, *"Kwa kuwa yote yaliotangulia kuandikwa, yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini."*

Wapo wale wanaosema Biblia iliandikwa na wanadamu waliokosea kuhusu kile walichoandika. Alafu wanakataa kwamba Mungu hakuweza kuongoza maandishi ya neno lake kwa wanadamu.

2 Tim. 3:15-17, *"Na ya kuwa tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yanaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu. Kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema."*

Agano la Kale inawakilisha maisha katika viwango vyote – mabaya na mazuri.

Kifungu hiki kinaongea kuhusu Mnara wa Babeli, uzao wa Shemu, wa Tera, nk.; lakini kwa wakati huu nataka kunakili misitari ya 27-32:

Mwanzo 11:27-32, *"Na hivi ndivyo vizazi vya Tera. Tera akamzaa Abramu, na Nahori, na Harani. Harani akamzaa Lutu. Harani akafa kabla ya baba yake Tera katika katika nchi aliyozaliwa, yaani, katika Uru wa Wakaldayo. Abramu na Nahori walijitualia wake. Jina la mkewe Abramu aliitwa Sarai, na jina la mkewe Nahori aliitwa milka, binti Harani, ambaye alikuwa baba wa Milka na wa Iska. Na Sarai alikuwa tasa, hakuwa na mtoto. Tera akamtwaa Abramu mwanawe, wakatoka wote katika Uru wa Wakaldayo, waende nchi ya Kanaani, wakafika mpaka Harani wakakaa huko. Siku za Tera zilikuwa miaka mia mbili na mitano; Tera akafa katika Harani."*

Tera anahamisha familia yake kutoka Uru wa Wakaldayo. Makazi yake yalikuwa ni Kanaani (kati ya Yordani na Bahari ya Mediterenian).

Hakuweza kufika: msitari wa 31, *"Tera akamtwaa Abramu mwanawe, na Lutu mwana wa Harani, mwana wa mwanawe, na Sarai mkewe, na mke wa Abramu mwanawe, wakatoka wote katika Uru wa Wakaldayo, waende nchi ya Kanaani, wakafika mpaka Harani wakakaa huko."*

Mnara wa Babeli na Uru vyote vilikuwa katika nchi ya sasa ambayo ni Iraki. Harani ilikuwa kaskazini mwa Uru na Kanaani ilikuwa magharibi mwa Uru. Hata ivyo, wafugaji wakisafiri na mifugo ilifuatia rutuba iliyotengenezwa na mto Yufreti. Ingekuwa ni kujiua kama wange jaribu kusafiri moja kwa moja magharibi hadi maili mamia ya ardhi, hasa na mifugo. Kama wange safari mwendo wa moja kwa moja hadi katika nchi ya Kanaani kupitia bonde lenye rutuba hadi kaskazini, wangekuwa wamesafiri kiasi cha maili 1,000. Harani ilikuwa kiasicha maili 500 kutoka Uru, na kiasi cha maili 500 kutoka Kanaani: NJIA YA MKATO!

Tera, kwa sababu ambazo hatuzijui, HAKUWEZA kupita njia ya mkato katika safari yake hadi Kanaani.

Watu wengi wako kama Tera. Wanajua wanapo paswa kwenda, au wanapoitaji kwenda, lakini wanafikia njia ya mkato. Wengi wanaishi katika "*nchi ya Harani*" katika mtazamo wa kiroho.

Walianza vizuri; walikuwa na maendeleo mazuri, lakini hapo ndipo walipofikia. Changa moto ni kusonga mbele; kufikia malengo.

Katika somo hili nataka tushirikiane baadhi ya ukweli juu ya lengo: Njia ya mkato si mbali vya kutosha.

Mwanzo mzuri hautoshi

Ndiyo, mwanzo mzuri ni muhimu, na inapaswa iwe sahihi.

Anayeshiriki katika riadha za mita 100 anatakiwa awe na mwanzo mzuri iwapo anatarajia kushinda. Mwanzo mzuri unamaanisha mengi kwake. Mtu aliyekulia kanisani anakuwa na mwanzo mzuri ukilinganisha na mtu anayekuwa mkristo baadaye katika maisha. Yule aliye lelewa kanisani kwa kawaida anakuwa hana tabia mbaya ambazo ni ngumu kuzivunja baadaye, tofauti na wale waliolelewa kwa njia ya kidunia.

Yohana 8:32-36, *"Tena <u>mtaifahamu kweli na hiyo kweli itawaweka huru</u>. Wakamjibu sisi tu wazao wake Ibrahimu, wala hatujawa watumwa wa mtu wakati wo wote; nawe wasemaje mtawekwa huru? Yesu akawajibu, Amin amin nawaambia, kila atendaye dhambi mi mtumwa wa dhambi. Wala mtumwa hakai nyumbani sikuzote; mwana hukaa siku zote. Basi mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli."*

Tukiifahamu kweli mapema katika umri mdogo tunaweza kuwa huru na makosa mengi yanayofanywa na hao ambao hawakulelewa katika mazingira ya kanisa.

Yoh. 3:1-5, *"Basi kulikuwa na mtu mmoja wa Mafarisayo, jina lake Nikodemo mkuu wa Wayahudi. Huyo alimjia usiku akamwambia, Rabi, twajua ya kuwa u mwalimu, umetoka kwa Mungu; kwa maana hakuna*

mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye. Yesu akajibu akamwambia, Amin amin, nakuambia, mtu asipozaliwa mara ya pili hawezi kuuona ufalme wa Mungu. Nikodemo akamwambia awezaje mtu kuzaliwa akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa? Yesu akajibu, Amin amin nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho hawezi kuuingia ufalme wa Mungu."

Kuwa katika mbio za Ukristo lazima tuwe "*katika Kristo*."

- Waef. 1:3, *"Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa Baraka zote za rohoni, katika ulimwengu war oho, ndani yake Kristo."*
- Wagal. 3:27, *"Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo."*

Ubatizo unamweka mtu katika mbio za Ukristo. Kama mtu hajabatizwa atatoa udhuru mwingi anazojua kwamba ameshinda mbio, lakini Mungu anakataa kanuni hiyo kwa sababu haikuwa mbio yake.

Hataivyo, lazima tuendelee na kuendelea.

- Ufu. 2:10, *"...Kuwa mwaminifu mpaka kufa name nitakupa taji ya uzima."*
- Waeb. 12:1-3, *"Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, tukimtazama Yesu mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu, ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu. Maana mtafakarini sana yeye aliyeyastahimili mapingamizi makuu namna hii ya watendao dhambi juu ya nafsi zao, msije mkachoka, mkizimia mioyoni mwenu."*

Hatuwezi kutarajia kushinda mbio kama tukibeba mizigo. Tuweke kando mizigo ya dunia hii kama tunatarajia kushinda mbio za Mungu. Kukimbia njia ya mkato kwenda mbinguni si mbali vya kutosha.

Kuudhuria ibada kanisani haitoshi. Kile tunacho sikia na kujifunza lazima iwekwe katika matendo.

Yakobo 1:18-22, *"Kwa kupenda kwake mwenyewe alituzaa sisi kwa neno la kweli, tuwe kama limbuko la viumbe vyake. Hayo mnajua ndugu zangu wapenzi. Basi kila mtu na awe mwepesi wa kusikia, bali si mwepesi wa kusema; wala kukasirika; kwa maana hasira ya mwanadamu haiitendi haki ya Mungu. Kwa hiyo wekeni mbali uchafu wote na ubaya*

uzidio, na kupokea kwa upole neno lile lililopandwa ndani, liwezalo kuziokoa roho zenu. Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu."

Wayahudi walifikiri wana kibali cha moja kwa moja hadi mbinguni kwa sababu walikuwa uzao wa Ibrahimu. Hawakufanya walichoambiwa kufanya na Mungu. Kristo akasema kutakuwa na kilio na kusaga meno wakijikuta hawata ungana na Ibrahimu mbinguni.

Njia ya Mkato ni adui wa...

Malengo yaliyofikiriwa.

Ni rahisi kuandika malengo yetu chini, tunapoanza, lakini badaye wengi wanafikia njia ya mkato. Mafanikio yanakuja baada ya kuhitimu.

Mhubiri. 7:8, *"Heri mwisho wa neno kuliko mwanzo wake, na mvumilivu rohoni kuliko mwenye roho ya kiburi."*

Wakristo wachanga wakatimwingine wanataka kubadilisha ulimwengu. Wanakatishwa tama wanapotaka matokeo muda huo uo. Mwisho unakuwa mzuri kuliko mwanzo.

Kiwango cha juu.

Chochote tufanyalo kwa jina la Kristo lazima iwe mafanikio yetu. Maisha yetu lazima yawe masafi na lazima tuwe na adabu njema. Math. 5:8, *"Heri wenye moyo safi maana hao watamwona Mungu."*

Neno linasema, "ni nini kibaya na njia ya mkato kimsingi?" Sikiliza Yesu:

Math. 6:24-25, *"Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili, kwa maana atamchukia huyu na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali. Kwa sababu hiyo nawaambieni msisumbukie maisha yenu, mle nini, au mnywe nini; wala miili yenu, mvae nini. Maisha je si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi."*

Kama ukijaribu kuishi katika sehamu mbili (Mungu na wanadamu) utajiuzulu vya Mungu.

Ukuwaji.

Kukuwa nusu haitoshi.

Waef.4:11-16, *"Naye alitoa wengine kuwa mitume na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapoufiki*

umoja wa imani na kumfahamu sana mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo; ili tusiwetena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja tukizifuata njia za udanganyifu. Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa Kristo. Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikamana kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo."

Wale waliowachanga katika mwili wa Kristo hawawezi kujizuia na upepo wa kila namna ya mafundisho ya kidini. Hawajajifunza kuchunguza kila kitu wanachosikia kuhusiana na mafundisho ya Mungu. Ndiyo sababu Paulo alimwambia kijana Timotheo kujifunza.

Katika mbio za ridhaa baadhi ya wanaridha hawasomi misitari ya kukimbilia vizuri an wanakimbia katika muelekeo ambao si sahihi. Wakati wanapogundua kosa wanakuwa wamepoteza mbio. Misitari hiyo hatakama imetengenezwa na mtu na haikuwa wazi hadi hao wanaofuata kukosea.

Lazima tusishindanie njia ya mkato.

Kuwa kama Kristo.

Yesu alimaliza kazi yake. Akasema, "*Imekwisha".* Alituachia mfano wa kufuata.

Ilikumaliza kituchochote vizuri inamchukua mtu kufanya kazi ngumu. Tumeumbwa kwa ajili ya kazi njema. 1 Wakor. 15: 58*, "Basi ndugu zangu wapendwa, mwimarike msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana sikuzota, kwa kuwa mwajua ya kwamba taabu yenu siyo bure katika Bwana."*

Kwa nini tunakaa kwa ajili ya njia ya mkato?

Kwa sababu wengine wanaogopa kuendelea zaidi.

Njia ya mkato ni rahisi. 2 Tim. 1:7*, "Maana Mungu hakutupa roho ya woga bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi."*

Paulo hakuchukua njia fupi. Aliongea kwa ujasiri mbele ya nyuso za hatari. Bado hakuogopa kile ambacho kingemtokea, hata angekufa akimtumikia Bwana, alijua maisha mazuri kuliko haya yanamsubiri. Akijua hilo linaweza kutupatia upendo na moyo wa kiasi licha ya hatari za dunia hii iliyoko mbele yetu.

Kwa sababu hamu ya safari imepotea.

Vitu vingine vilikuwa mhimu zaidi kwao – kazi zao, familia zao, na vitu vingine vya kuvutia. Vitu ambavyo vinawaachanisha na kazi yao ya kumtumikia Bwana

Ufu. 3:14-22, *"Na kwa malaika wa kanisa lililoko Laodikia andika; haya ndiyo anenayo yeye aliye amina, shahidi aliyemwaminifu na wa kweli, mwanzo wa kuumba kwa Mungu. Nayajua matendo yako yakuwa hu baridi wala hu moto; ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto. Basi. Kwa sababu una uvuguvugu wala hu baridi wala moto nitakutapika utoke katika kinywa change. Kwa kuwa wasema mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi. Nakupa shauri ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako upate kuona. Wote niwapendao mimi nawakemea na kuwarudi, basi uwe na bidii ukatubu. Tazama nasimama mlangoni nabisha, mtu akiisikia sauti yangu na kuufungua mlango nitaingia kwake name nitakula pamoja naye, nay eye pamoja name. Yeye ashindaye nitampa kuketi pamoja name katika kiti change cha enzi kama mimi nilivyo shinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi. Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa."*

Walikuwa vuguvugu. Kazi zao zilikuwa za mkato.

Ufu. 3:19, *"Wote niwapendao mimi nawakemea na kuwarudi, basi uwe na bidii ukatubu."*

Kwa sababu ya mvuto wa wengine kwetu.

Mtindo wetu unatuvutia (ubosi, uongozi nk) hivyo tunafikiria kile ambacho wengine wanafanya na hiyo ni kawaida na ni sahihi. 1 Wakor. 15:33, *"Msidanganyike mazungumzo mabaya uaribu tabia njema."* Kristo ni mtindo wetu.

Kwa sababu ya uvivu.

Wengine hawapendi kufanya kazi.

- Mithali 15:19, *"Njia ya mtu mvivu ni kama boma la miiba; bali mapito yao wenye unyofu hufanyika njia kuu."*
- Mithali 24:30-32, *"Nalipita karibu na shamba la mvivu, na shamba la mizabibu la mtu asiye na akili. Kumbe! Lote pia lilmemea miiba; uso wake ulifunikwa kwa viwavi; na ukuta wake wa mawe*

umebomoka. Ndipo nilipoangalia na kufikiri sana; naliona nikapata mafundisho."

- Mithali 12:27*, "Mtu mvivu hapiki mawindo yake, bali mwenye bidii anazo malizenye dhamani."*

Nilimpa mtu kazi ya kusafisha kitu Fulani. Akakataa akisema alikuwa na mlolongo wa kazi nyingi. Hataivyo, alifanya kazi ya kukusanya pesa katika mitaa. Hakutaka kufanya kazi; ilikuwa ni rahisi kuomba omba ela.

Redio ya Seattle iligundua kwamba asilimia 95% ya waombaji walikuwa hawafai. Walikuwa kamilifu kufanya kazi; walichagua tu mfumo huo wa maisha kwa sababu ilikuwa rahisi badala ya kufanya kazi.

Kwa sababu ya ujeuri.

Hosea 4:6-8*, "Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa; kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa; mimi name nitakukataa wewe, usiwe kuhani kwangu mimi, kwa kuwa umeisahau sheria ya Mungu wako, mimi name nitawasahau watoto wako. Kadiri walivyozidishwa, na kadiri iyo hiyo walinitenda thambi nami nitageuza utukufu wao kuwa aibu. Hujilisha dhambi ya watu wangu, hujifurahisha moyo kwa uovu wao."*

Kijana! zungumzia mvuto wa dhambi zako! Mungu alisema kama ukikataa maarifa yake. Atawakataa watoto wako pia. Kwa nini hivi? Watawezaje kujifunza mambo ya Mungu kama baba zao hawaku wafundisha?

Huwezi kufanya usichokijua. 2 Tim. 2:15*, "Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari ukitumia kwa halali neno la kweli."*

Kwa sababu ya ugumu wa moyo

"Nitaifanya kesho." Hapana, hebu na tuifanye leo. Yoshua 24:15, *"...chagueni leo ni nani mtakae mtumikia...."* Hatujui kesho itakuwaje.

Kila mkristo yuko safarini kwenda mbinguni.

- Waeb. 11:16*, "Lakini sasa waitamani nchi iliyo bora, yaani ya mbinguni. Kwa hiyo Mungu haoni haya kuitwa Mungu wao; maana amewatengenezea mji."*

- Waeb. 13:14*, "Maana hapa hatuna mji udumuo, bali twautafuta ule ujao."*

Lazima tusikomee njia ya mkato. Mwanzo mzuri haitoshi. Katika mpira wa pete, kuingia katika hatua Fulani haiongezi mbio nyingine katika kufunga.

Njia ya mkato ni adui wa imani yetu. Lazima tuondoe vitu vinavyotuzuia. Usikae Harani, kama Tera alivyofanya.

Jichunguze mwenyewe. Uko wapi? Endelea kwenda. Na wote tukutane katika musitari wa kumalizia.

Ufu. 2:10, *"Usiogope mambo yatakayokupata tazama huyo ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufa, name nitakupa taji ya uzima."*